



BENKI KUU YA TANZANIA

MFUMO WA MALIPO WA TISS

Nini maana ya TISS?

TISS ni mfumo wa malipo makubwa na ya haraka unaoendeshwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kirefu cha TISS ni “Tanzania Interbank Settlement System”. Mfumo huu unatumika kulipia malipo mbalimbali makubwa na ya haraka. Pia mfumo huu unawezesha ulipanaji wa malipo mbali mbali ya kibenki yaliyofanyika kuititia kwenye mfumo wa hundi, mfumo wa malipo wa kielektroniki (EFT) , mifumo ya malipo yatokanayo na mifumo mingine kama vile mifumo ya Malipo ya Kadi pamoja na Malipo katika Masoko ya Fedha. TISS inamilikiwa na Benki Kuu.

Nani watumiaji wa TISS?

Watumiaji wa TISS ni mabenki ambayo kwa sasa yamefikia 33 hapa nchini Watumiaji hawa hutuma na kupokea malipo yao wenyewe na kwa niaba ya wateja wao pia. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pia ni mtumiaji wa mfumo huu katika kukusanya mapato ya serikali.

Mfumo wa TISS unafanyaje kazi?

Watumiaji wa mfumo wa TISS pia ni wanachama wa mtandao wa SWIFT ambao unaaminika kuwa mtandao salama kabisa wa kimataifa katika kutuma ujumbe wa kifedha. Wanachama wa TISS wanatuma na kupokea ujumbe wa malipo kuititia mtandao huu. Mteja akitaka kutuma fedha kuititia mfumo wa TISS anatoa maelekezo kwa benki yake kupeleka fedha kwenye akaunti ya mteja mwingine anayetumiwa katika benki yake. Baada ya kupokea maelekezo ya malipo, benki husika hutuma maelekezo ya malipo kwa mtumiwa kwa kutumia mfumo wa TISS baada ya kujiridhisha kuwa mtumaji ana fedha za kutosha katika akaunti yake. Benki inayopokea malipo hayo ikishapata huo ujumbe, inapaswa kuweka fedha katika akaunti ya muhusika ndani ya “MASAA MAWILI “tangu kupokea maelekezo ya kulipa.

Je, mfumo huu unahakikishaje kuwa mteja anayetumiwa fedha anaingiziwa fedha hizo kwenye akaunti yake mara moja kwa kutumia mfumo wa malipo wa TISS (Tanzania Interbank Settlement Systems)?

Kanuni za Uendeshaji za Mfumo wa Malipo wa TISS (TISS Rules and Regulations) zinaelekeza fedha zimfikie mtumiwa si zaidi ya **MASAA MAWILI** tangu benki husika ilipopokea maagizo ya kulipa fedha hizo ikiwa maelekezo ya malipo yako sahihi.

Tofauti na TISS kuna mifumo gani mingine ya Malipo?

Mifumo mingine ya malipo iliyopo ni:

- Mfumo wa malipo wa hundi, “Automated Cheques Clearing System”. Mfumo huu hutumiwa na mabenki katika kubadilishana hundi.
- Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki (Electronic Fund Transfer). Mfumo huu hutumika kupitisha malipo makubwa ambayo hugawanywa katika mafungu madogomadogo kama vile mishahara, malipo baada ya kustaafuli (pension funds) n.k.
- Malipo ya kadi yanayotumiwa na miamala (ATMs), na ving’amuzi vyta manunuzi (POS)
- Kufanya malipo, kuhamisha fedha au kufanya manunuzi kwa njia ya Mtandao (Internet Banking).
- Kutuma au kutumiwa fedha kutoka au kwenda nchi mbalimbali duniani kwa kutumia huduma za Western Union, MoneyGram na Coinstar.
- Kutuma au kutumiwa fedha ndani ya nchi kwa huduma za Shirika la Posta kama vile Postal Order, Money Order na Money Fax.
- Kutuma fedha kwa njia ya simu za mkononi kama vile M-pesa, Z-pesa na ZAP.

Nini faida za TISS ?

- Malipo kupitia mfumo wa TISS yanafanyika papo kwa papo, hivyo basi mtumiwa fedha ana uhakika wa kupata fedha siku hiyo hiyo. Ni njia rahisi ya kutuma fedha zenye thamani kubwa na kwa haraka zaidi.
- Mfumo wa TISS unapunguza athari ambazo huweza kutokea kama fedha zitatumwa kwa njia za kawaida. Athari hizi ni pamoja na wizi, kughushi na ucheleweshwaji wa malipo.
- Mfumo huu una unafuu katika Malipo yake kwani kila ombi (transaction) la kutuma malipo halipaswi kutozwa zaidi ya shilingi elfu kumi (Tzs 10,000/=).